# Aliyetoa jina la Tanzania afariki nchini Uingereza ..Uk.3

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.37 Tanzania Bora JUMATANO Machi 05, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100




# Waziri Mavunde atangaza neema sekta ya madini

HABARI UK.2

- >> Atoa nafasi kwa sekta binafsi kufanya kazi pamoja na serikali
- >> Awakumbuka wachimbaji wadogo na kuagiza Stamico kufanikisha upatikanaji vifaa
- >> Eneo la kufanyia utafiti sasa kuongezwa zaidi ili kazi ifanyike kwa upana zaidi
- >> Ni mpango wa serikali kunufaisha wachimbaji wadogo kufaidika na jasho lao 777






## Makala awataka Chadema wasipotoshe watanzania

NA MWANDISHI WETU

KATIBU wa Uenezi na Mafunzo wa CCM CPA Amos Gabriel Makala alisema kuwa viongozi wa Chamdema kuanzia Mwenyekiti wao Tundu Lisu na wenzake wote, hakuna hata mmoja mwenye ubavu wa kuzuia kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu nchini hapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa chama na jumuiya ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es salaam

Inaendelea Uk. 2

## Dk. Biteko asisitiza matumizi ya nishati safi barani Afrika

HABARI UK.2



# WAZIRI MAVUNDE ATANGAZA NEEMA SEKTA YA MADINI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Madini Mh. Anthony Mavunde amezikaribisha nchini Tanzania Kampuni za Utafiti wa madini kushirikiana na serikali katika kutimiza malengo ya Mining VISION2030 ambayo imejikita katika kufanya utafiti wa kina wa madini kufikia eneo la ukubwa wa asilimia 50 kufikia mwaka 2030.

Mh. Mavunde ameyasema hayo jana Toronto, Canada wakati akihutubia kikao cha Mawaziri wa Madini kutoka nchi mbalimbali duniani,Kampuni za Utafiti na Uendelezaji Migodi na Asasi za kiraia.

ìSerikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia S. Hassan imeweka mazingira wezeshi ya kiuwekezaji,hivyo ni fursa kubwa ya Kampuni za Utafiti kuja kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika mkakati wake wa kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa kina wa madin i.

Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Madini, inatekeleza mpango wa utafiti wa madini wa kina kutoka eneo la utafiti wa kina la asilimia 16 kufikia eneo la asilimia 50 kufikia mwaka 2030.

Kwa kuwa Tanzania ni kisiwa cha amani, uongozi imara na mazingira mazuri ya kiuwekezaji nichukue fursa hii kuwakaribisha wadau kuungana na serikali katika mpango wake huu wa utafiti wa kina wa madini nchini kwa kuwa serikali peke yake haiwezi kufanya kwa eneo lote hivyo sekta binafsi ni muhimu katika kufikia azmaìAlisema Mavunde

Awali akiwa katika mabanda ya maonesho ya vifaa vya Madini,akiongozana na Balozi wa Tanzania nchini Canada Mh. Joseph Sokoine na wataalamu wa Wizara ya Madini,Waziri Mavunde amemuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO Dkt. Venance Mwasse kuangalia namna ya upatikanaji wa vifaa vya utafiti wa awali wa madini ili wakati wachimbaji wadogo wakipata huduma ya uchorongaji kuwepo pia vifaa vya awali vya kusaidia kuonesha maeneo yanayopaswa kuchorongwa.




# MAKALA AWATAKA CHADEMA WASIPOTOSHE WATANZANIA

NA MWANDISHI WETU

KATIBU wa Uenezi na Mafunzo wa CCM CPA Amos Gabriel Makala alisema kuwa viongozi wa Chamdema kuanzia Mwenyekiti wao Tundu Lisu na wenzake wote, hakuna hata mmoja mwenye ubavu wa kuzuia kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu nchini hapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa chama na jumuiya ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es salaam CPA, Makalla amesema kuwa CHADEMA inafanya Makosa makubwa kuwahadaa wananchi wasijiandikishe kwa madaikuwahakutakuwa na uchaguzi.

Amesisitiza kuwa uchaguzi utafanyika kwa mujibu wa sheria na katiba, na kwamba madai ya CHADEMA kwamba ìNo Reform, No Electionî ni propaganda zisizo na msingi na hivyo zipuuzwe.

Vilevile amewataka Wenyeviti wa Serikali za Mitaa waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika Novemba Mwaka jana, kutanguliza huduma na utumishi kwa wananchi wao, kwani waliomba utumishi na wakiwakilishe chama kama walivyoaminiwa.

# ALIYETOA JINA LA TANZANIA AFARIKI NCHINI UINGEREZA

NA MWANDISHI WETU

MOHAMMED Iqbal, aliyekuwa msomi na mchambuzi wa masuala ya kisiasa, alikuwa miongoni mwa Watanzaia walioshiriki katika mijadala muhimu kuhusu muungano wa Tanganyika na Zanzibar mefariki jana nchini Uingereza alikohamia tangu mwaka 1968.

Katika harakati hizo, alitoa pendekezo la jina ìTanzania,î ambalo lilitokana na mchanganyiko wa majina ya Tanganyika na Zanzibar, na hatimaye likakubaliwa rasmi na viongozi wa wakati huo, akiwemo Mwalimu Julius Nyerere.

Katika mahojiano na waandishi wa habari miaka kadhaa nyumba Mohammed aliwahi kutoa ufafanuzi kuhusiana na jinsi alivyobuni jina hilo loa Tanzania.

Alisema kwa muongozo wa Mungu alichukua herufi tatu za kwanza za Tanganyika (TAN) na herifi tatu za Zanzibar (ZAN) na kisha akaongeza (I) kutoka kwa jina lake Iqbal na Imani yake katika Uislamu. Hatimaye akakumbuka uhusiano wake na madhehebu ya Ahmadiyya na akaongeza (A) ili kuheshimu madhehebu hayo, na hivyo TANZANIA ikatokea.

Mohammed Iqbal alizaliwa katika kipindi cha ukoloni Agosti 8, 1944 na alihusika kwa kiasi kikubwa katika mijadala ya utaifa na harakati za ukombozi wa Tanganyika.

Alikuwa mtu mwenye uelewa wa kina kuhusu historia, utambulisho wa kitaifa, na umuhimu wa mshikamano wa bara na visiwa.

Mnamo mwaka 1964, Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuunda taifa jipya. Kulikuwa na mjadala wa jina gani lingeweza kubeba dhana ya umoja wa nchi hizo mbili, na hapo ndipo Mohammed Iqbal alipoleta wazo la ìTanzaniaîójina lililopokelewa kwa furaha na hatimaye kuwa rasmi.

Katika maisha yake, Iqbal aliendelea kuwa mchangiaji mkubwa katika mijadala ya maendeleo ya kitaifa na umuhimu wa utambulisho wa Tanzania. Kupitia mchango wake, jina ìTanzaniaî limebaki kuwa alama ya mshikamano wa Watanzania na kiashiria cha historia ya taifa.

Kwa kifo cha Mohammed Iqbal, taifa limepoteza mtu muhimu aliyetoa mchango mkubwa katika historia yake. Serikali, viongozi wa kisiasa, wasomi, na wananchi kwa ujumla wanaendelea kuomboleza kifo chake huku wakikumbuka mchango wake usiosahaulika.

# WAJAWAZITO NA WATOTO WAPATA HUDUMA ZA AFYA

NA MWANDISHI WETU

WANAWAKE na wajawazito na watoto 178 wamefanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya moyo katika zoezi la upimaji wa magonjwa hayo linalofanyika jijini Arusha katika maonesho ya kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Wanawake.

Upimaji huo wa siku nane unafanywa na wataalamu wanawake wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha katika viwanja vya TBA Kaloleni karibu na Mnara wa Mwenge mkabala na Makumbusho ya Taifa Arusha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha daktari bingwa wa magonjwa ya moyo kwa watoto na Mkuu wa Kitengo cha Utoaji wa Huduma Bora wa Taasisi hiyo Dkt. Naiz Majani alisema leo ni siku ya tatu tangu wameanza kufanya upimaji huo na wameona wanawake 88, wajawazito 42 na watoto 48.

Dkt. Naiz alisema katika upimaji huo wamewapima wanawake wajawazito kipimo cha Echokadiografia ya moyo wa mtoto aliyepo tumboni, kipimo hicho kinamsaidia mama kutambua afya ya moyo wa mtoto wake kabla hajajifungua kwani ni muhimu kwa wajawazito kufanya uchunguzi wa afya ya moyo wa mtoto awapo tumboni ili wataalamu wajue namna ya kutatua tatizo la mtoto kama anashida katika hatua za awali.

ìWanawake na watoto tuliowapima na kuwakuta na matatizo mbalimbali ya moyo walikuwa 29 kati ya hao watu wazima 26 na watoto watatu, sita kati yao watu wazima wakiwa wanne na watoto wawili tumewapa rufaa ya kuja kufanyiwa uchunguzi zaidi na kupata matibabu ya kibingwa katika taasisi yetu iliyopo Upanga jijini Dar es Salaamî, alisema Dkt. Naiz.

ìKati ya wajawazito 42 tuliowafanyia kipimo cha Echokariografia ya moyo wa mtoto aliyepo tumboni watoto watatu tumewakuta na shida ya moyo na tumeandika barua maalumu ya rufaa kwenda katika hospitali watakazo jifungulia na tumechukuwa taarifa zao na tarehe watakazo jifungua, tutaendelea kuwafuatilia ili kujua maendeleo ya watoto hao ikiwa ni pamoja na kuanzishiwa matibabu mapemaî.

ìTupo hapa kwa lengo la kupima watoto ambao wanadalili za magonjwa ya moyo au wazazi wanaotaka kufahamu afya za watoto wao, kikubwa zaidi taasisi yetu imekuja kufanya uzinduzi wa kampeni maalumu ya kugundua magonjwa ya moyo kwa watoto wakiwa tumboni,kampeni hii ni muhimu sana kwani kugundua mtoto ana maradhi gani akiwa tumboni kutasaidia kaanzishiwa matibabu sahihi na kwa harakaî, alisema Dkt. Naiz.

Dkt. Naiz alisema katika matibabu ya maradhi ya moyo wanayotoa JKCI wamebaini magonjwa mengi ya moyo kwa watoto kama yangegundulika mapema watoto hao wangetibiwa mapema na kupona.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mara baada ya kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya moyo wakazi wa Arusha walifurahi kwa huduma waliyoipata na kusema kuwa imewapa nafasi ya kupima na kutambua afya za mioyo yao. Willian Mute mkazi wa Kaloleni alisema alikuwa na tatizo la moyo kwenda mbio baada ya kufanyiwa vipimo vya katika hospitali ya Mount Meru alikutwa na tatizo la shinikizo la juu la damu na kuanzishiwa dawa ila baada ya kusikia kuna wataalamu wa moyo wako jijini Arusha akaona atumie nafasi hiyo kupima tena afya ya moyo wake.

ìNimepima kipimo cha kuangalia jinsi moyo wangu unavyofanya kazi nimekutwa uko sawa na sasa hivi nasubiri kufanyiwa kipimo cha mfumo wa umeme wa moyo. Nashukuru sana kwa huduma hii kwani nimeipata bila malipo yoyote yaleî, alisema Mute.

ìNashukuru sana nimepima afya ya moyo wa mtoto wangu aliyepo tumboni namshukuru Mungu yuko salama, nawaomba kinamama wenzangu ambao ni wajawazito watumie nafasi hii kupima na kutambua afya za mioyo ya watoto wao ili kama watakutwa na shida ya moyo waanze matibabu mapema mara baada ya kuzaliwaî, alishukuru Mariam Juma mkazi wa Mianzini.



# DUA MAALUM KWA DK SAMIA YAFANYIKA

NA MWANDISHI WETU

MAMIA wameshiriki dua ya pamoja maalumu ya kumuombea Rais wa Jamhuri ya muungano Tanzania Dr Samia na taifa kwa ujumla wilayani Makete mkoani Njombe na kisha kutumia sadaka zilizotolewa na waombaji kwa kutoa msaada kwa waye mahitaji maalumu wakiwemo wazee, yatima na walemavu wanaoishi katika wilaya hiyo.

Awali mbunge wa Makete Festo Sanga na Mkuu wa wilaya ya Njombe Juma Sweda walisema kuwa Mungu ameweka maono kwa viongozi wa nchi katika kutumikia watu, hivyo kuna haja ya kuombea viongozi wa nchi watekeleza maono ili wapate hekima na maarifa ya kuongoza vyema hasa katika kuelekea uchaguzi mkuu ujao, hivo inatumazimu kufunga na kuomba ili upite kwa amani.

Wamesema wameguswa kufanya maombi maalumu ya Rais na, ili uchaguzi uwe na amani ya nchi kwasababu Mungu ndiyo mlinzi wa mwanadamu.

Kwa upande wa viongozi wa dini akiwemo Shekh wa wilaya ya Makete Anwari Sanga amesema katika dua hiyo, wamechangia sadaka ya kusaidia wenya uhitaji ambapo Mbunge Sanga amechangia shilingi laki 5 .

Nae Rodrick Sanga mwenyekiti wa Chadema Makete amesema tujitahidi kueonyesha upendo kwa makundi yote na kwamba itikadi za kisiasa zisiwe sababu ya kubaguana.

# DK. BITEKO ASISITIZA MATUMIZI YA NISHATI SAFI BARANI AFRIKA



NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema licha Bara la Afrika kuwa na mchango mdogo katika uchafuzi wa hali ya hewa, nchi za Afrika bado zimekuwa mstari wa mbele katika kuendesha ajenda ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuijumuisha katika mifumo yao ya kisheria na udhibiti ikiwemo ya kuhakikisha kuwa nchi zinahama kutoka kwenye matumizi ya nishati chafu na kutumia nishati safi ili kuiepusha dunia na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Dkt. Biteko amesema hayo jana wakati akifungua Mkutano wa awali kuelekea Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAPCEí25) litakaloanza rasmi kesho ambapo mkutano huo wa awali ulilenga kujadili mipango na mikakati itakayopelekea matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kupikia na vyombo vya usafiri (CNG).

Amesema mkutano wa EAPCEí 25 ni jukwaa muhimu kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wadau wengine kujadili mipango na mikakati kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi hasa ikizingatiwa kwa sasa dunia inapambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na shughuli za binadamu huku tafiti za kisayansi zikionesha kuwa viwango vya utoaji wa hewa ya ukaa vimeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu kufanyika kwa Mapinduzi ya Viwanda.

ì Nataka nichukue nafasi hii kuwaomba wote muutumie mkutano huu kujadili masuala ambayo yatatufanya sisi wana Afrika Mashariki, tuweze kuhama kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyokuwa safi kwenda kwenye matumizi ya nishati iliyosafi, lazima mtambue kwamba mkutano huu wa awali haujatokea kwa bahati mbaya, kama jamii tunayo kazi ya kufanya ya kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi kwenda matumizi ya nishati safi.î Amesisitiza Dkt.Biteko

Ameeleza kuwa, sheria nyingi zinazopitishwa kwa sasa barani Afrika zinahimiza uchumi wa kijani, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuwa na maendeleo endelevu ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa upande wake imeandaa Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi ikiwa ni uthibitisho wa dhamira ya kanda hiyo katika kushughulikia tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na kuhimiza matumizi ya nishati safi.

Ametaja baadhi ya athari za mabadiliko ya tabia nchi kuwa ni pamoja na ukame mkali, mafuriko, kupotea kwa viumbe hai, kupungua kwa vyanzo vya maji safi, kuyeyuka kwa barafu, na ongezeko la magonjwa yanayohusiana na tabianchi kama vile saratani ya ngozi.

Dkt.Biteko ameeleza kuwa suala la mabadiliko ya tabia nchi linatiliwa mkazo pia katika ngazi ya dunia na hii imepelekea kuwepo kwa mikataba mbalimbali ya kimataifa ukiwemo wa Kyoto, Montreal na Paris ambapo nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinaandaa na kutekeleza mikakati inayohusiana na tabianchi ikiwemo kujikita katika matumizi ya nishati safi zisizochafua mazingira ikiwemo Gesi Asilia.

Kuhusu upatikanaji umeme amesema Afrika ndiyo Bara linalokabiliwa na upungufu mkubwa wa nishati duniani, ambapo asilimia 75 ya watu wanaokosa nishati duniani wanapatikana barani humo lakini juhudi zinafanyika ili kuwezesha upatikanaji wa nishati na hili lilithibitishwa kupitia Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati uliofanyika Tanzania Januari mwaka huu ambao uliweka mikakati ya kuongeza upatikanaji wa umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo mwaka 2030 ambayo ni hatua muhimu kuelekea mabadiliko ya kinishati.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia amesema mabadiliko yanahitajika ili kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi kwani idadi kubwa ya watu barani Afrika bado wanategemea kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia akitolea mfano nchini Tanzania, takriban asilimia 81 ya kaya zinatumia kuni na mkaa kama vyanzo vyao vikuu vya nishati ya kupikia, hali inayosababisha upotevu wa misitu wa takriban hekta 469,420 kila mwaka akitanabaisha kuwa mwelekeo huo wa kutisha unahitaji hatua za haraka na za pamoja ili kuendeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia barani kote.

Amesema katika kukabiliana na changamoto hiyo nchini Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni kinara wa ajenda nishati safi ya kupikia kitaifa na kimataifa kwa ujumla amechukua hatua madhubuti kwa kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Nishati Safi ya Kupikia (2024ñ2034) ambao unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Aidha amesema kuwa, matumizi ya gesi asilia kama nishati ya kuendeshea vyombo vya usafiri pia ni muhimu katika kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi akieleza kuwa Serikali ya Tanzania inaendelea kuboresha mazingira kwa wawekezaji binafsi kushiriki katika ujenzi wa Vituo vya Gesi Asilia Iliyoshindiliwa (CNG) na kuboresha sera na mifumo ya udhibiti.

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga kwa upande wake amesema mkutano huo wa awali unaweka msingi wa Kongamano la 11 la Mafuta kwa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki litakaloanza kesho Machi 05, 2025.

ìSiku ya leo kutakuwa na mada mbalimbali zitakazozungumzwa, ambazo zitakuwa na majadiliano yatakayoweka msingi kwa ajili ya mkutano mkuu utakaoanza kesho na kufanyika kwa siku tatu, mkutano huu ni muhimu katika kuwaweka wadau pamoja na kujadiliana masuala ya msingi ambayo yatazisaidia Nchi za jumuia ya Afrika Mashariki katika Sekta ya Mafuta na Gesi.î Amesema Kapinga

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuwa mkutano huo wa Mafuta na Gesi unaenda sambamba na Maonesho ya bidhaa za mafuta na gesi pamoja na kazi mbalimbali zinazofanyika katika sekta miongoni mwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ameeleza kuwa, Mkutano umelenga kuangalia namna bora ya kuhama kutoka kwenye nishati zinazochafua mazingira kwenda kwenye nishati safi zisizochafua mazingira ikiwa ni kampeni ya dunia ambayo imetokana na malengo ya dunia ya kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2050 hadi 2060 dunia iwe imeweza kuhamia kwenye nishati safi kwa kiasi kikubwa.



# SERIKALI YATOA LESENI KUBWA YA UCHIMBAJI MADINI YA KINYWE KWA

NA MWANDISHI WETU

TANZANIA imeandika historia mpya katika Sekta ya Madini baada ya Machi 3, 2025, Serikali kutoa Leseni Kubwa ya Uchimbaji (Special Mining Lisence-SML) wa Madini ya Kinywe (Graphite) kwa Kampuni ya EcoGraf Limited kupitia Mgodi wa Epanko Graphite, uliopo Kijiji cha Epanko Wilaya ya Mahenge, Mkoani Morogoro.

Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa Serikali wa kuboresha Sekta ya Madini hapa nchini sambamba na kuongeza thamani kwa maliasili zake ikiwemo za madini ambako Mradi huo unatarajiwa kuleta mapinduzi makubwa katika uchumi, viwanda, ajira, na nafasi ya Tanzania katika soko la kimataifa la nishati safi.

Katika taarifa yake kwa umma, Mkurugenzi Mtendaji wa EcoGraf, Andrew Spinks amesema kuwa Serikali ya Tanzania ilifanya tathmini ya kina ya maendeleo ya Mradi wa Epanko na kwamba Kampuni hiyo inatoa shukraniza dhati kwa Rais wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde, kwa msaada wao na kwa kuidhinisha utolewaji wa leseni hiyo.

*Mapato Makubwa kwa Serikali na Uwekezaji Endelevu

Serikali ya Tanzania itanufaika na kodi na tozo mbalimbali zitakazotokana na shughuli za mgodi wa Epanko. Mapato hayo yanaweza kuelekezwa katika miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa shule, hospitali, barabara, na miradi mingine ya kijamii.

Licha ya dola milioni 850 sawa na shilingi trilioni 2.1 zinazotarajiwa kulipwa na kampuni hiyo kama kodi, gawio, ada, mrabaha na ununuzi wa huduma na bidhaa tofauti katika kipindi cha kuendesha shughuli zake, inakadiriwa itachangia zaidi ya dola bilioni 2.5 sawa na shilingi trilioni 5.6 kwenye pato la Taifa (GDP).

*Mapinduzi ya Sekta ya Viwanda na Ongezeko la Thamani kwa Madini Kinywe (Graphite)

ìHatua hii inafanya Mradi wa Epanko kuwa mradi mkubwa zaidi ya madini kinywe barani Afrika ambao upo tayari kuendelezwa. Akiba ya madini kinywe ya Epanko (Ore Reserve) inakadiriwa kuwa tani 290.8 Mt, ikitoa uhakika mkubwa katika uendelezaji wa madini, ubora wa madini yatakayosafishwa, mambo ambayo ni muhimu katika kuamua bei sokoniî imesema taarifa hiyo.

Epanko Graphite itahakikisha kwamba uchakataji wake unafanyika hapa nchini kabla ya kusafirishwa nje huku Tanzania ikijitengenezea nafasi ya kuwa kitovu cha uzalishaji wa madini hayo yenye thamani ya juu, ambayo ni malighafi muhimu kwa utengenezaji wa betri za magari ya umeme na mifumo ya kuhifadhi nishati mbadala.

ìUtolewaji wa Leseni Kubwa ya Uchimbaji (SML) ni hatua muhimu katika maendeleo ya Epanko na sharti kuu kwa mchakato wa ufadhili, ambao utasaidia hatua ya kwanza ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa kiwanda cha kuchenjua grafiti chenye uwezo wa kuzalisha tani 73,000 kwa mwaka.î Imeongeza taarifa hiyo.

*Tanzania kuwa Kiungo Muhimu Katika Sekta ya Nishati Safi Duniani

Dunia inashuhudia mageuzi makubwa ya kuachana na nishati ya mafuta na kuelekea kwenye nishati safi. Magari ya umeme na mifumo ya kuhifadhi nishati ya jua na upepo vinahitaji betri bora zenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi chaji kwa muda mrefu. Madini ya Kinywe (Graphite) ni moja ya malighafi muhimu zaidi katika utengenezaji wa betri hizo, na mradi wa Epanko utaiweka Tanzania katika nafasi ya kimkakati kama mtoa huduma wa malighafi hii kwa masoko ya makubwa ya Ulaya, Asia, na Amerika Kaskazini.

Kwa kuzingatia kuwa Madini ya Kinywe ya Tanzania ni ya kiwango cha juu, nchi inaweza kuwa moja ya wazalishaji wakubwa duniani, hivyo kuongeza nguvu ya Tanzania katika soko la kimataifa la betri za umeme. Ndani ya kipindi kifupi inaweza kuongeza nafasi ya Tanzania katika diplomasia ya kiuchumi, kwani nchi zilizoendelea zinauhitaji mkubwa wa malighafi hiyo.

*Ajira na Uboreshaji wa Maisha ya Watanzania

Moja ya manufaa makubwa ya mradi wa Epanko ni kuongeza fursa za ajira kwa maelfu ya Watanzania. Mradi huo hautahusisha tu uchimbaji wa madini, bali pia usindikaji wake, usafirishaji, na huduma za kusaidia shughuli za mgodi kama vile chakula, usafiri, na ulinzi. Hii inamaanisha kuwa wataalamu wa migodi, wahandisi, madereva, mafundi, wachimbaji, na wafanyabiashara wa huduma watafaidika moja kwa moja na mradi huu.

Kwa kuzingatia kuwa mgodi huu unapanua eneo lake kutoka 9.6 km≤ hadi 18.9 km≤, inamaanisha kuwa kuna fursa kubwa zaidi za ajira kwa Watanzania wengi, hasa kutoka jamii zinazozunguka mgodi. Zaidi ya hayo, kampuni ya EcoGraf inatarajia kutoa mafunzo kwa vijana wa Kitanzania ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za mgodi kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Kwa upande mwingine, sekta ya biashara za ndani pia itanufaika, kwani kutakuwa na ongezeko la mahitaji ya bidhaa na huduma kama vile malazi, chakula, vifaa vya ujenzi, na vifaa vya uchimbaji. Hii itaimarisha uchumi wa ndani na kuchochea maendeleo katika sekta mbalimbali.

Mradi wa Epanko Graphite siyo tu fursa ya kiuchumi kwa Tanzania, bali ni hatua muhimu kuelekea mapinduzi ya sekta ya madini na viwanda. Kupitia ajira, maendeleo ya viwanda, uuzaji wa bidhaa zenye thamani ya juu, na nafasi ya kimataifa kwenye sekta ya nishati safi, Tanzania inajiimarisha kama mshindani mkubwa katika soko la kimataifa la graphite.

# MBUNGE APIGA JEKI UJENZI WA SHULE

NA MWANDISHI WETU

MBUNGE wa Jimbo la Lulindi, Issa Mchungahela, ametoa msaada wa mifuko ya saruji 600 katika Kata ya Mpindimbini, kwa ajili ujenzi wa miundombinu ikiwamo vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na matundu ya

Akikabidhi msaada huo wa mifuko ya saruji mbele ya viongozi wa kata hiyo, pamoja na wananchi katika mkutano wa hadhara, uliofanyika katika kijiji cha Mpindimbini Kata ya Mpindimbini.

Alisema akiwa kama Mbunge wa Jimbo la Lulindi, ataendelea kushirikiana na wananchi wa jimbo hilo na hasa katika kuhakikisha maendeleo yanapatikana.

Mchungahela ameeleza kwamba mifuko hiyo 600 ya saruji amejitoa baada ya kuona katika baadhi ya maeneo ndani ya jimbo hilo kuna changamoto ya miundombinu hafifu katika maeneo muhimu ikiwamo kwenye shule.

"Nimetoa mifuko hii ya saruji 600 kwa lengo la kutatua changamoto ya miundombinu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vyumba vya madarasa kwa shule za awali na maeneo mengine ya msingi," alisema Mchungahela.

Alisema mifuko ya saruji inakwenda katika vijiji mbalimbali ndani ya Kata ya Mpindimbini, kwa mgawanyo ili kila sehemu yenye changamoto ya miundombinu ikasaidie kutatua.

Mchungahela alisema mifuko 200 kati ya hiyo 600, itatumika kwenye ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Mpindimbi, huku mifuko 100 itatumika kwenye ujenzi wa nyumba ya mwalimu shule ya msingi Mpindimbi.

Aliongeza kuwa mifuko 100 pia inakwenda kutumika kwenye ujenzi wa darasa la awali kitongoji cha Muungano.

Mchungahela alielezea kuwa mifuko 100 ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa shule tarajali Mapale, huku mifuko 100 mingine kwa ajili ya umaliziaji wa boma la Zahanati Kijiji cha Kachepa.

Aidha mbunge huyo aliwapongeza wananchi wa vijiji hivyo, kwa kushiriki kikamilifu shughuli za maendeleo kwa kuibua miradi mbalimbali, ikiwamo ujenzi wa shule tarajali na zahanati ambazo zitapunguza umbali wa wananchi kufuata huduma hizo.

Mchungahela akihutubia mkutano wa kijiji cha Mapale, alisema kuwa serikali ina mpango madhubuti wa uchimbaji wa bwawa ambalo litasaidia wananchi wa maeneo hayo, ambayo wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha umwagiliaji kufanya shughuli zao

# BIL 300 KUIDHINISHWA KWA MAENDELEO MANYARA



NA MWANDISHI WETU

MKOA wa Manyara wenye Halmashauri zake saba imeomba kuidhinishiwa Sh302.9 bilioni za mpango wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026.

Katibu Tawala msaidizi (Mipango na Uratibu) wa ofisi ya mkuu wa mkoa wa Manyara, Lusungu Mwilongo, akisoma rasimu ya mpango wa bajeti ya mkoa huo mjini Bahati kwenye kikao cha kamati ya ushauri (RCC) amesema makisio ya bajeti ni Sh302.9 bilioni.

> Kwa ujumla, skimu hiyo itakuwa mkombozi kwa wengi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Toufiq, ambaye pia alipongeza NSSF kwa kuboresha.

Mwilongo amesema fedha hizo zinajumuisha Sh224.1 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh78.7 bilioni kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Amesema ofisi ya mkoa huo imepangiwa Sh10.8 bilioni, halmashauri ya mji wa Babati Sh32 bilioni, wilaya ya Babati Sh59.1 bilioni na Hanangí Sh56.1 bilioni.

Amesema Kiteto imepangiwa kiasi cha Sh38.7 bilioni, wilaya ya Mbulu Sh38.7 bilioni, Mbulu mji Sh29.3 bilioni na Simanjiro sh37.5 bilioni.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga amesema kupitia serikali ya awamu ya sita mkoa huo umepiga hatua kwenye sekta mbalimbali.

Sendiga amesema maeneo tofauti ya mkoa wa Manyara yamepiga hatua katika sekta ya elimu, maji, afya na miundombinu mbalimbali.

ìTunaishukuru mno serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ilivyofanikisha miradi mbalimbali kwenye mkoa wetu wa Manyaraî, amesema Sendiga.

Mkazi wa mji wa Babati, John Ombay amesema pamoja na kupitishwa kwa mpango huo wa bajeti, jamii inaona maendeleo yanayofanyika.

Ombay amesema shule mpya zinajengwa Manyara, vituo vipya vya afya na zahanati kwenye vijiji hivyo kuonyesha kwa macho maendeleo yanavyopatikana.

ìPamoja na kuwa bado kuna changamoto mbalimbali kwa jamii ila maendeleo tunaona ikiwemo suala la usambazaji maji hasa vijijini hivyo hatuna budi kuipongeza serikali kwa kutimiza vyema wajibu wake,î amesema Ombay.

Mkoa wa Manyara ulioanzishwa mwaka 2002 una ukubwa wa kilomita za mraba 44,522 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 una watu 1,893,000 katika wilaya tano zenye vijiji 440.

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakukuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

## MAWASILIANO

JAMVI MEDIA GROUP




*Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya Faru 18 iliyofanyika katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mkoani Arusha jana.*

# UCHAMBUZI

## Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI
DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# TANZANIA YAPOKEA FARU WEUPE 18



NA MWANDISHI WETU

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mara ya kwanza imepokea Faru Weupe 18 kutoka Afrika Kusini kwa lengo la kuimarisha uhifadhi nchini.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika katika Hifadhi ya Ngorongoro, mkoani Arusha, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, amesema kuwa mradi wa kupandikiza faru hao ni hatua muhimu katika juhudi za uhifadhi nchini.

"Mradi huu wa kupandikiza Faru Weupe ndani ya hifadhi ya Ngorongoro ni jitihada za serikali katika kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori na unatekelezwa kwa mara ya kwanza kupitia makubaliano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kampuni ya AndBeyond," amesema Chana.

Ameeleza kuwa katika makubaliano hayo, kampuni ya AndBeyond imechukua jukumu la kuwezesha upatikanaji na usafirishaji wa faru hao 18 kutoka Afrika Kusini kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili inatarajiwa kuleta faru wengine 18 ili kufikisha jumla ya faru 36, ambapo wengine watawekwa katika maeneo mengine ya uhifadhi nchini.

Chana amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za dhati za kukuza na kuimarisha sekta ya uhifadhi, ikiwa ni pamoja na mradi huu wa kupandikiza faru weupe.

Aidha, amebainisha kuwa Faru Weupe ni miongoni mwa wanyamapori walioko hatarini kutoweka na hivyo wameorodheshwa katika makundi yanayolindwa chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo Hatarini Kutoweka (CITES).

"Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za kimataifa, hususan za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kwa kulinda wanyamapori hawa katika mazingira ya asili badala ya kuwafuga kwenye mashamba maalum au bustani," ameongeza Chana.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mbali na kuimarisha uhifadhi, Faru Weupe pia watatumika katika elimu ya jamii kuhusu usimamizi wa wanyamapori, kuendeleza tafiti za kisayansi na kuboresha mbinu za uhifadhi wa spishi hiyo.

Kwa upande wake, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Dk. Elirehema Doriye, amesema kuwa kupokelewa kwa faru hao ni uthibitisho wa dhamira ya Tanzania katika kulinda spishi zilizoko hatarini kutoweka.

"Faru hawa watachangia juhudi za kimataifa za uhifadhi, kuongeza fursa za tafiti na kitaalamu, kukuza utalii, na kuinua uchumi wa jamii. NCAA imejipanga kuhakikisha usalama wao," amesema Dk. Doriye.

Naye, Mwakilishi wa Viongozi wa Kimila kutoka Afrika Kusini, iNkosi Zwelinzima Gumedeunywano, amesema kuwa lengo la kutoa faru hao kwa Tanzania ni kusaidia juhudi za uhifadhi na kuongeza uzalishaji wa faru katika Afrika Mashariki.

"Tafiti zinaonyesha kuwa Faru Weupe watastawi na kuzaliana vizuri katika eneo la Ngorongoro," amesema Gumedeunywano, akisisitiza kuwa Afrika Kusini iko tayari kushirikiana na Tanzania katika juhudi za uhifadhi wa spishi hiyo.

Picha mbalimbali za matukio wakati Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alipofuturisha Watoto Yatima na Watoto wenye mahitaji Maalum, Ikulu Jijini Dar es Salaam, juzi.









Picha mbalimbali za matukio wakati Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alipofuturisha Watoto Yatima na Watoto wenye mahitaji Maalum, Ikulu Jijini Dar es Salaam, juzi.

# NLD YATAKA WASIMAMIZI UCHAGUZI WENYE WELEDI




NA MWANDISHI WETU

CHAMA cha National League for Democrats (NLD), kimetangaza kuanza kwa mchakato wa ndani ya chama wa kuwapata wagombea wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais kuelekea Uchaguzi Mkuu, utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Aidha chama hicho kimetangaza neema kwa wagombea wanawake, kuwa hawatotoa ada yoyote wakati wa kuchukua fomu, lengo ni kuwapa fursa ya kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi.

Akizungumza mapema leo na waandishi wa Habari, Katibu mkuu wa NLD Taifa ,Doyo Hassan Doyo, amesema, chama hicho kimelenga kusimamisha wagombea katika majimbo yote ya Uchaguzi kuanzia Udiwani, Ubunge pamoja na nafasi ya Rais,

"Chama chetu kitashiriki Uchaguzi Mkuu, hivyo kwakutambua hilo, leo tunatangaza rasmi kuwa ,chama kimefungua milango ya kuanza mchakato wa kuwapata wagombea wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais, hivyo watu wote wenye sifa wanakaribishwa kushiriki, ili ukidhi sifa ya kushiriki mchakato huu ni lazima uwe Mwanachama hai wa Chama chetu," aliongeza Doyo

Doyo alisema kuwa, kwaupande wa wagombea Wanawake hawatolipa ada yoyote wakati wa mchakato wa kuchukua fomu,

"Chama chetu, kwa mapenzi mema kabisa, na kwakuona umuhimu wa akinamama, tumeamua kuwa, wanawake wote watakaojitokeza kugombea nafasi za uongozi ndani ya chama chetu, hawatolipa ada yoyote ya fomu, hii itasaidia kuongeza hamasa na kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za Udiwani, Ubunge na Rais" Alisisitiza Doyo

> Amesema changamoto zingine zinazowakabili wanawake wenye ulemavu, kama vile ukatili wa kijinsia, unyanyapaa, na ubaguzi katika jamii.

Aliongeza kuwa katika kikao cha Kamati Kuu ya Chama hicho Februari 23, mwaka huu, chama hicho kilianzimia kuwa kabla ya Uchaguzi Mkuu ni lazima kufanyike mikutano ya hadhara na ndani ili kupata wagombea wenye uwezo pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi 'INEC' nilazima iweke wasimamizi wa Uchaguzi wenye weledi, ili uchaguzi uwe huru na haki.

Hicho ni chama cha pili cha siasa kilichotangaza kushiriki uchaguzi Mkuu kabla ya hapo CCM ambacho ni chama tawala nacho kilithibitisha kushiriki tukio hilo la kikatiba.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Mgombea Mwenza wa Urais Tanzania Bara, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, amewahimiza wanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi kuendelea kujipanga vyema ili kuhakikisha chama kinashinda Uchaguzi nafasi za Ubunge na Udiwani kwa kuzingatia sera na maadili.

Ilikuwa ni katika kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya hiyo jijini Dodoma, Dkt. Nchimbi alisisitiza kuwa CCM ni chama kinachojikita katika sera na maendeleo, si katika matusi au kejeli.

"Chama chetu kimefanya mambo makubwa kwa maendeleo ya taifa. Tunapaswa kuendelea kusimamia hoja zenye mashiko na si kutumia lugha zisizofaa. Tunapaswa kuwa mfano wa kuheshimu watu na kuzungumzia maendeleo yanayoonekana," alisema.

Aidha, alieleza kuwa serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanikisha mambo mengi ambayo yanaweza kuwahamasisha wananchi kuendelea kukiamini chama.

"Tunayo mengi ya kuwaambia Watanzania kuhusu maendeleo yaliyofikiwa, hatuna sababu ya kutumia lugha za kejeli. Hayo tuwaachie wale wasiokuwa na hoja za msingi," aliongeza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi Taifa, Fadhili Maganya, alisema kuwa ujio wa Dkt. Nchimbi katika kikao hicho ni ishara ya heshima kwao.

"Uwepo wako hapa umetupa faraja kubwa. Tumekukaribisha ili usikilize mawazo yetu na kutushauri. Hii ni historia, kwani sisi ndiyo jumuiya ya kwanza kuketi na wewe tangu uteuliwe kuwa mgombea mwenza," alisema Maganya.

Kikao hicho kilitoa fursa kwa viongozi wa Umoja wa Wazazi kujadili masuala muhimu yanayohusu ustawi wa jumuiya na mchango wake katika mustakabali wa chama kuelekea uchaguzi ujao.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi aliyasema haya kwenye Kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Baraza Kuu la Umoja wa Wazazi, Jumuiya ya CCM, ambacho alialikwa na kushiriki akiwa mgeni maalum, leo Jumamosi tarehe 8 Februari 2025, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

"Katika kikao chetu cha hivi karibuni, chama chetu kiliazimia kuwa ni lazima tufanye mikutano ya hadhara kwakipindi hiki ili tupate wagombea wenye uwezo, lakini pia kwa upande wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi 'INEC' ni lazima iweke wasimamizi wa Uchaguzi wenye weledi ili Uchaguzi uwe huru na haki, na usiwe na dosari," alisisitiza Doyo

# GAZA KUJENGWA UPYA KWA GHARAMA YA DOLA B.20



NA MWANDISHI MAALUM

VIONGOZI wa nchi za Kiarabu wanaokutana Cairo,Misri kujadili jinsi ya kujenga upya Gaza wameidhinisha mipango ya kujenga makaazi mapya laki mbili kwa gharama ya dola bilioni ishirini.

Mpango huo hautawaondoa Wapalestina katika makazi yao.

Mpango huo pia unataka uchaguzi ufanyike katika maeneo yote ya Palestina katika kipindi cha mwaka mmoja.

Viongozi hao wameiomba jumuiya ya kimataifa na asasi za kifedha kujitolea kufadhili mpango huo. Umoja wa Mataifa unakadiria kuwa gharama ya kuujenga upya ukanda wa Gaza ni zaidi ya dola bilioni hamsini.

Nchi za kiarabu zimekuwa zikikabiliwa na shinikizo la kujanamapendekezombadala na yale yaliyotangazwa na Rais wa Marekani Donald Trump ya kutaka kudhibiti Gaza na kuhamisha Wapalestina wa Gaza hadi nchi jirani,pendekezo ambalo limepingwa vikali na nchi hizo za kiarabu na jumuiya ya kimataifa.

Kundi la wanamgambo la Hamas limetaka viongozi hao wanaohudhuria mkutano huo wa kilele kuepusha kuondolewa kwa wapalestina wa Gaza.

Hamas inasema inatumai kuwa viongozi wa kiarabu watakuwa na wajibu muhimu na utakaokomesha janga la kibinadamu lililosababishwa na kukaliwa kimabavu kwa ukanda wa Gaza.

Marekani ilikuwa imependekeza Wagaza wahamishiwe nchi jirani za Misri na Jordan.

Mkutano huo unajiri huku kukiwa na mkwamo kati ya Hamas na Israel kuhusu hatua inayofuata juu ya hatma ya makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyofikiwa kati ya pande hizo mbili tarehe 19 Januari.

Baada ya awamu ya kwanza ya makubaliano hayo kuisha mwishoni mwa juma lililopita bila ya muafaka ya namna gani yataendelezwa,Waziri mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alitangaza misaada ya kiutu izuiwe kuingia ukanda wa Gaza.

Hii ni habari njema kwa wahanga wa vita katika eneo hilo lililoshuhudia uharibifu mkubwa wa miundombinu na vifo vya mamia kwa maelfu ya wakazi wake, lakini hivi karibuni hali ilianza kuwa yenye matumaini baada ya Malori yaliyosheheni chakula, vifaa vya makazi na dawa yameingia Ukanda wa Gaza kwa kiwango cha takriban 600 kwa siku tangu mapatano ya kusitisha vita kuanza tarehe 19 Januari ikiwa ni idadi kubwa zaidi kuliko ile iliyoruhusiwa wakati wa mapigano yaliyosababishwa na mashambulizi ya kigaidi ya Hamas dhidi ya Israel tarehe 7 Oktoba 2023.

Jumatano pekee, zaidi ya malori 800 yalikubaliana kutoa bidhaa za kuokoa maisha kwa Gaza, imesema OCHA huku shirika la Umoja wa Mataifa la msaada kwa wakimbizi wa Palestina, UNRWA, likisema kuwa limefikia watu milioni 1.5 kwa usambazaji wa chakula tangu kuanza kutekelezwa kwa makubaliano ya kusitisha vita na lina bidhaa za kutosha kufikia idadi iliyobaki ya watu wa Gaza.

Tangu vikosi vya Israel kujiondoa kutoka sehemu za mpaka wa Netzarim unaotenganisha kaskazini na kusini mwa Gaza, inakadiriwa kuwa watu zaidi ya 586,000 wamevuka kwenda kaskazini, huku zaidi ya 56,000 wakiwa wamehamia kusini, zimeeleza ripoti za wahudumu wa kibinadamu wa Umoja wa Mataifa.

Licha ya ongezeko kubwa la msaada, bado haijatosha kutoa msaada wa haraka ambao zaidi ya watu milioni mbili wakazi wa Gaza wanahitaji.

Hii itatokea tu pale bidhaa za kibiashara zitakaporudi kuingia kwenye Ukanda wa Gaza, wamesema wahudumu wa kibinadamu mara kwa mara, ikiwemo Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto UNICEF ìMsaada mwingi umeingia. Tumepanua wigo wa juhudi zetu haraka iwezekanavyo katika wiki tatu zilizopita za makubaliano ya kusitisha vita, lakini kwa hakika hatuwezi kufuta mateso ya miezi 15 kwa wiki tatu,î amesema Meneja wa Mawasiliano wa UNICEF, Tess Ingam, akizungumza na UN News.

Ameongeza kuwa “Kunahitajika kuwa na msaada zaidi unaoingia kwa muda mrefu pia tunahitaji bidhaa za kibiashara kuingia ili masoko yaweze kujazwa. Tunahitaji sekta ya fedha na benki kuanzisha tena huduma ili watu waweze kununua bidhaa hizo za kibiashara. Kuna mengi yanayohitaji kufanyika haraka ili kusaidia kurejesha hali ya kibiashara katika Ukanda wa Gaza.”

UNICEF pia imeonya kuwa timu zake haziwezi kurekebisha kwa haraka uharibifu uliofanywa na jeshi la Israeli kwa kutumia silaha nzito na mashambulizi ya anga kote Gaza.

Huduma za msingi za umma zimesambaratishwa na zinahitaji vifaa ambavyo bado haviruhusiwi kuingia katika eneo hilo.

“Tunahitaji kuhakikisha kwamba vitu fulani ambavyo kwa sasa vimewekewa vikwazo vya kuingia Gaza vinaweza kuingia, kwa mfano, mabomba ya kutengeneza mifumo ya maji, jenereta za kuendesha pampu za maji,” amesema Bi. Ingam, mara baada ya kumaliza jukumu la tathmini la wiki mbili katika eneo hilo.

“UNICEF inahitaji makubaliano haya ya kusitisha vita yashike kwa kiasi kikubwa kwetu kama ilivyo kwa watoto wa Gaza,” amesisitiza akiongeza kuwa “Kama washirika wote wa kibinadamu, tunaweza kufanya kazi yetu bora kuokoa maisha ya watoto na kuwapa ulinzi na msaada tunapokuwa hatufanyi kazi chini ya mashambulizi ya moto wa moja kwa moja.”

Akizungumza moja kwa moja na UN News, Bi. Ingam amesema vipaumbele vya shirika hilo vitatu ni kutoa maji, kuboresha huduma za afya na lishe, na kuwasaidia watu kustahimili majira ya baridi.

“Tumejikita kuhakikisha kwamba maji yanarudi tena, hasa katika maeneo ambapo mifumo ya maji imeharibiwa vibaya, mabomba yameharibiwa, visima vimeharibiwa kaskazini na katika Rafah, kwa hivyo tunajaribu kurejesha maji kwa kufanya marekebisho na pia kuanzisha usambazaji wa maji kwa malori ili familia ziweze kupata maji mara moja.”

# JUHUDI ZINAHITAJIKA ZAIDI KUOKOA MAISHA YA MAJERUHI GOMA

NA MWANDISHI WETU

GHASIA za hivi karibuni huko Goma, Kivu Kaskazini, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, DRC, kuanzia mwishoni mwa mwezi Januari zimeongeza mahitaji ya huduma za afya. Ili kukabiliana na hali hiyo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya Duniani (WHO) limechangia vifaa muhimu vya matibabu, ikiwa ni pamoja na mahema na vitanda, kwa vituo vya afya ili kusaidia katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa. Kupitia video iliyoandaliwa na WHO.

Video iliyorekodiwa kuanzia mwanzoni mwa mwezi huu wa Februari 2025 hadi majuzi, inaanzia juu angani kuonesha madhari ya mji wa Goma, kisha inashuka chini mtaani ambako pilika za siku zinaendelea.

Na sasa video hiyo inatupeleka katika Hospitali ya Rufaa ya Goma. Dkt Jean Bruno ambaye ni Mkuu wa Ofisi ya WHO Kivu Kaskazini anaingia katika moja ya mahema yaliyoko hapa yakitumika kama wodi za muda za WHO na anaonekana akizungumza na wagonjwa wanaopata huduma hapa. Yuko katika hema la wanawake.

Dkt. Jean Bruno baada ya kuzungumza na wagonjwa, sasa ametoka ndani, anazungumza kwa matumaini akisema,

"Katika jiji la Goma kwa sasa. Utulivu unarejea polepole. Tunaweza pia kuona kuwa shughuli za kijamii na kiuchumi zimeanza kurejea taratibu."

Video hii inaonesha sasa mafundi chini ya usimamizi wa maafisa wa shirika la Msalaba Mwekundu na WHO wakisimika mahema mengine zaidi katika maegesho ya magari ya hospital hii ya rufaa ya Kivu Kaskazini. Vyuma na maturubai meupe vinatolewa katika makasha makubwa ya mbao, vinasimamishwa na kuunda mahema ambayo kila moja linatoa nafasi ya kuweka vitanda 20 vya wagonjwa, kumi kila upande.

Wahudumu wa afya katika hospitali ya Goma watoa msaada kwa waathiriwa wa mapigano katika siku za hivi majuzi.

Dkt Jean Bruno na Dkt Gaston Lubin wanajadiliana jambo. Dkt Gaston Lubin, ni Mganga Mkuu katika Hospitalini hapa anaeleza kwa nini kinachoendelea hapa ni muhimu,

"Kwa sababu kulikuwa na majeruhi wengi, ilihitajika kuongeza nafasi kwa kusimika mahema. Lakini mahema yaliyowekwa pia yana magodoro. Hili limewezesha kupokea wagonjwa wengi na kutoa huduma zinazofaa kulingana na aina za majeraha yaliyokuwepo."

Bada ya hapo Dkt Jean Bruno anaingia katika hema jingine, sasa ni la wanaume, anazungumza na mmoja wa wagonjwa anayeitwa Zulu Augustin.

Zulu Augustin analo la kusema, "Hapa hospitalini, tunaishi vizuri, tunasimamiwa vyema na kulindwa vizuri. Tunapewa kila kitu kwa ajili ya kula, dawa, na kila kitu kiko sawa."

Zulu Augustin ni majeruhi, ana majeraha kuanzia usoni hadi miguuni, anaeleza kilichosababisha majeraha kwenye mwili wake akisema, "Kulikuwa na vipande vya mabomu vilivyoingia na pia risasi. Tuliitoa risasi, lakini haikugonga mfupa. Ndio, kwa sasa hali ni nzuri."

Dkt Jean Bruno, kama nilivyoeleza awali yeye ni Mkuu wa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya Duniani Kivu Kaskazini bado yuko hapa anazungumza na wagonjwa na baada ya kutoka ndani anaeleza changamoto akisema,

"Ukweli ni kwamba hatuna rasilimali za kutosha, hasa rasilimali za kifedha, kutoa msaada wote unaohitajika. Kuna changamoto tunazoweza kuzingatia, kama vile kusaidia wagonjwa kwa ajili ya mwendelezo wa matibabu, lakini pia utambuzi, utafiti na urejeshaji wa wagonjwa, hasa wale wenye magonjwa ya kuambukiza, kama vile waliokuwa na surua, kipindupindu au mpox, ambao walijikuta katika jamii. Hivyo basi, utafutaji wa haya pia ni changamoto kwa sasa."

Umoja wa Mataifa kupitia mashirika yake na wadau wake wengine wameendelea kujitahidi kuhudumia jamii ya mashariki mwa DRC japo katika mazingira magumu kutokana na hali tete ya usalama inayotatiza pia usafiri kwa wafanyakazi na vifaa.



Inaendelea Uk. 13

# JUHUDI ZINAHITAJIKA ZAIDI KUOKOA MAISHA YA MAJERUHI GOMA

Inatoka Uk. 12

Tangu mapigano ya hivi karibuni katika ya jeshi la DRC na waasi wa M23 yalipopamba moto, yamechochea joto zaidi la changamoto za wananchi wa eneo hilo.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa AntÛnio Guterres, akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa 58 wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, huko jijini Geneva, Uswisi, ameshutumu vikali wachochezi wa vita wanaodharau sheria za kimataifa, sheria za kibinadamu za kimataifa na Katiba ya Umoja wa Mataifa na akasisitiza matumizi ya diplomasia katika kutatua migogoro ulimwenguni.

Hivi karibuni Muungano wa waasi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Alliance Fleuve Congo (AFC), unaojumuisha waasi wa M23, umetangaza kuwa tayari kushiriki mazungumzo na serikali ili kusitisha mara moja mapigano mashariki mwa nchi, msemaji wa kundi hilo amesema.




Lawrence Kanyuka amechapisha ujumbe kwenye ukurasa wake wa mtandao waa X, akitangaza kuwa AFC imejitolea kwa suluhisho la mazungumzo ya mgogoro.

Amesema hatua hiyo inalenga kuwezesha utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa hivi karibuni katika mkutano wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), pamoja na mkutano wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika. Kanyuka amesema:îMaazimio haya yanatoa wito wa kusitisha mapigano kati ya pande husika na mazungumzo ya kisiasa kati ya Serikali ya Kongo na AFC/ M23. Tunatumaini kuwa serikali, wakati huu, itaheshimu na kutekeleza kikamilifu maazimio haya.î

Katika taarifa tofauti, muungano wa waasi uliishutumu serikali ya DRC na wanamgambo washirika wao kwa kuendelea kufanya mashambulizi ya ardhini na angani dhidi ya raia katika maeneo kadhaa, hasa Uvira na Minembwe katika jimbo la South Kivu.

Hayo yanajiri wakati ambao Tanzania jana Jumatatu, ilikuwa ni mwenyeji wa mkutano wa kikanda, kufuatilia matukio ya nyanjani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kuchukua hatua zinazohitajika za kukabiliana na mgogoro huo.

Mkutano huo unahudhuriwa na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Katika mapigano ya hivi karibuni, waasi wa M23 wameteka miji miwili mikubwa ya DRC ambayo ni Goma na Bukavu katika eneo lenye utajiri wa madini la mashariki mwa nchi hiyo.






# SIMBA NA YANGA ZAJICHIMBIA DAR

>> Inatoka uk. 16

zimekuwa zikisalia katika Jiji la Dar es Salaam huku kila timu ikijifua kambini kwake.

Inadaiwa kuwa utaratibu wa kuzitoa timu nje ya Jiji umekuwa ukipotea polepole kutokana na mabadikiko ya benchi la ufundi na hata wachezaji wa kigeni ambao wamekuwa wakishinda kuelewa mantiki yake.

Inadaiwa kuwa safari ya kuzitoa nje ya Dar timu hizo mara nyingi zilikuwa zikihusishwa na masuala ya ushirikina ambayo kwa sasa yanazidi kupoteza mvuto ndani ya klabu hizo.

# KARIA ARIDHIA ULIPAJI KODI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania-TFF, Bw. Wallace Karia, amekubali mapendekezo ya Serikali na kuahidi kuwa suala la ulipaji kodi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Aidha ameahidi kuwa watalichukulia kwa uzito suala la Kodi katika michezo yote ya mpira wa miguu inayosimamia na Taasisi hiyo.

Kauli hiyo imetolewa katika kikao cha majadiliano kati yake na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Na (Mb) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi. Kikao hicho pamoja na masuala ya kodi walijadili maendeleo na changamoto zinazoikabili sekta ya michezo hususan mpira wa miguu nchini. Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, Serikali imeipongeza TFF na Bodi yake ya Ligi, kwa kusimamia kwa weledi masuala ya maendeleo ya soka na kulileteа Taifa heshima kubwa barani Afrika kiasi cha kupewa jukumu la kuandaa mashindano ya CHAN na AFCON.

Pia serikali ilikubaliana na namna tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo inavyoweza kutumika kuhamasisha uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari, kupitia kampeni ya kudai na kutoa risiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Majadiliano hayo yaliwashirikisha viongozi wa juu wa Wizara ya Fedha, akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, Bw.Yusuph Mwenda, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania- TFF, Bw. Wallace Karia, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Bw.. Almas Kasongo, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi zinazosimamia michezo nchini.





# P-SQUARE 'Mapacha' ndani ya mgogoro!-5

LOGOS, NIGERIA

Ni lazima ieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, "aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. "Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza."

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. "Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kwa kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha."

# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'

# Tamasha la muziki 'Kadanse ya Mama' yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.


Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.

Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz 'Wanamsondo ngoma' ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.





UK. 15

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA

MICHEZO

JUMATANO Machi 05, 2025

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz


# Simba na Yanga zajichimbia Dar



NA MWANDISHI WETU

KWA kawaida mambo yaliyokuwa yakitarajiwa huko nyuma kila inapokaribia mechi kubwa inayozikutanisha timu kongwe za Simba na Yanga, wachezaji, viongozi hulikimbia Jiji la Dar es Salaam na kwenda nje kwa ajili ya kufanya maandalizi.

Mara nyingi Simba ilishuhudiwa ikikimbilia Kisiwani Zanzibar na Yanga mara chache ilikuwa ikielekea Kisiwani Pemba au mikoa ya karibu na Dar es Salaam, Morogoro au Bagamoyo mkoa wa Pwani.

Lakini kadri siku zinavyozidi kwenda utaratibu huo umekuwa ukiondoka polepole na hivi sasa timu hizo

Inaendelea Uk.14

# WASEMAJI SIMBA, YANGA WAFUNGWA MIDOMO

NA MWANDISHI WETU

ZILE kejeli pamoja na tambo zilizozoeleka kusikika kila inapokaribia mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga katika hali isiyokuwa ya kawaida zimezimika huku mashabiki wakibaki ndiyo wanaoendeleza majibizano vijiweni.

Habari ambazo gazeti hili limezipata zimedai kuwa ukimya huo umetokana na Maafisa wa Habari wa Klabu hizi Ahmed Ali wa Simba na Ali Kamwe wa Yanga kuitwa na Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la soka Tanzania TFF.

Hata hivyo Waandishi wa habari waliofuatilia taarifa hizo hawakupata majibu baada ya Wasemaji hao kutoka katika kikao hicho na kukataa kuzungumza chochote kilichojiri.

Uchunguzi wa gazeti hilo umebaini kuwa pamoja na mambo mengine huenda wanahabari hao waliopewa majukumu ya kuzizungumzia klabu hizo kubwa, wamepigwa pini kutokana na mara nyingi kukiuka miiko pale

Inaendelea Uk.14



# GUARDIOLA AMPIGIA HESABU STRAIKA WA UINGEREZA



LONDON, UINGEREZA

HAKUNA ubishi kuwa Kocha wa Manchester City Pep Guardiola ana mpango kabambe wa kuboresha kikosi chake, hivyo jambo la muhimu kwake ni kuhakikisha anasajili nyota watakaoweza kuvaa uhusika wakuichezea klabu hiyo yenye hadi kubwa duniani.

Kama ndiyo hivyo basi, kinachoonekana mbele yake

Inaendelea Uk.14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM